TANZANIA COALITION ON DEBT AND DEVELOPMENT (TCDD)

HALI YA ELIMU NA AFYA NA CHANGAMOTO ZAKE NCHINI TANZANIA MWAKA 2014

NOVEMBA 2015

www.tcdd.or.tz

SHUKRANI

Kitabu hiki cha hali ya afya na elimu ni mwendelezo wa tafiti ambazo Mtandao wa Madeni na Maendeleo Tanzania (TCDD) imekuwa ikizifanya tangu mwaka 2001 katika sekta za afya na elimu. Kitabu hiki kinaainisha hatua zote za mchakato mzima wa ufuatiliaji, umuhimu, malengo, njia, sampuli na zana za utafiti. Kitabu pia kinatoa matokeo ya utafiti kwenye wilaya kumi na mbili (12) ambapo utafiti huu umejikita katika kufuatilia utekelezaji wa mpango wa MKUKUTA awamu ya pili ambao umeishia mwaka 2015 katika wilaya za Rungwe, Mufindi, Magu, Bahi, Mkuranga, Kishapu, Lindi, Biharamulo, Bunda, Kigoma Vijijini, Songea Vijijini na Newala. Kitabu hiki kinachambua matokeo hayo kutoka katika shule za Sekondari 120 na vituo vya afya 60 kama sampuli wakilishi ya sekta nzima katika wilaya hizo 12.

Shukrani za dhati ziwaendee wote waliohusika kikamilifu katika kukamilisha kazi hii kama ifuatavyo; Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya zote ambazo zimehusika kikamilifu katika utafiti huu, Wakuu wa Wilaya zote, Maafisa Elimu wa Wilaya na Waganga Wakuu wote wa Wilaya. Pia tunawashukuru Walimu Wakuu, matabibu na wadau wengine wote.

Kwa namna ya pekee tunapenda kuyashukuru mashirika wanachama wa TCDD hasa yaliyohusika kikamilifu katika utafiti huu katika Wilaya zao ambazo ni Tanzania Home Economics Association (TAHEA), Tambani Rural Community Development Fund (TARUCODEFU), Christian Council of Tanzania (CCT), Sustainable in Development Issues (SDI), Elimisha, Tanzania Diamonds and Gemstone Polishers Association (TDGPA), Lindi Non- Governmental Organization Network (LINGONET), Facilitation for Integrated Development and Relief Services (FAIDERS), Kigoma and Ujiji Non Governmental Network (KIUNGONET), Poverty Alleviation Organization (PAO), Faidika Wote Pamoja (FAWOPA) na Foundation Help.

Shukrani pia zimwendee Ndugu Boniface Komba ambaye ameandaa na kuweka pamoja taarifa hii kwa wilaya zote 12, Ndugu Jane Mwabulambo ambaye pia amefanya kazi ya kuboresha kitabu hiki katika hatua zote. Wote kwa ujumla wao walitoa mchango mkubwa katika kuboresha na kuchapisha kitabu hiki ambacho sio tu kwamba kitawasaidia watanzania na watunga sera kwa ujumla bali kitumike kama sehemu ya utetezi na uchechemuzi katika kuboresha huduma ya afya na elimu nchi nzima.

Hebron Mwakagenda
Mkurugenzi Mtendaji
Novemba 2015

YALIYOMO

Shukrani i
Yaliyomo ii
Vifupisho v

SURA YA KWANZA
UTANGULIZI 1
1.0. Msingi wa mradi wa utafiti 1
1.1. Ushiriki wa asasi za kiraia katika maendeleo 1
1.2. Njia za utafiti 1
1.3. Sampuli 1
1.4. Zana za ukusanyaji takwimu 2
1.5. Baadhi ya mambo muhimu yaliyoangaliwa kwenye utafiti huu 2

SURA YA PILI
2.0. MATOKEO YA UTAFITI KATIKA SEKTA YA ELIMU 3
2.1. Wilaya na idadi ya shule zilizohusika katika utafiti huu 3
2.2. Uwiano wa Udahili wa wanafunzi wa kike na kiume katika shule za sekondari 3
2.3. Kiwango cha ufaulu mtihani kidato cha nne na waliojiunga kidato cha tano 4
2.4. Uwiano wa walimu kwa wanafunzi 6
2.5. Hali ya miundombinu mashuleni 6
2.6. Umbali anaotembea mtoto kwenda shule mwaka 2015 8
2.7. Mafanikio 9
2.8. Changamoto 9
2.9. Mapendekezo 9

SURA YA TATU
3.0. MATOKEO YA UTAFITI KATIKA SEKTA YA AFYA 10
3.1. Hali ya afya kutokana na utafiti uliofanywa kwenye wilaya 11
3.2.Vifo vya watoto wachanga (Infanty Mortality Rate) 11
3.3. Vifo vya watoto wachanga chin ya miaka mitano (Underfive Mortality Rate) 12
3.4. Vifo vya akina mama wajawazito wakati na baada ya kujifungua 13
3.5. Changamoto 14
3.6. Mapendekezo 14

SEHEMU YA NNE
UFUATILIAJI WA MRADI WA 2011-2014 15
4.0. UTANGULIZI 15
4.1. Sekta ya elimu 15
4.2. Uwiano wa idadi ya walimu kwa wanafunzi 15
4.3. Miundombinu ya shule imeboreshwa 15
4.4. Idadi ya wanafunzi kwa madaraja ya ufaulu katika mtihani wa kidato cha nne 17
4.5. Mapendekezo ya TCDD 18

5.0. SEKTA YA AFYA KATIKA WILAYA..... 18
5.1. Vifo vya watoto wadogo chini ya mwaka 1..... 18
5.2. Miundombinu ya afya 20
5.3. Vifo vya watoto chini ya miaka 5 20
5.4. Mapendekezo ya TCDD..... 21

Orodha ya Majedwali

Jedwali Na 1: Idadi ya shule zilizohusika 3
Jedwali Na 2: Linabainisha uwiano wa jinsi ya kike na kiume Katika shule za sekondari..... 4
Jedwali Na.3: Ufaulu wa wanafunzi mwaka 2014 5
Jedwali Na 4: Uwiano wa walimu na wanafunzi mwaka 2014 6
Jedwali Na 5: Umbali anaotembea Mtoto kwenda Shuleni 8
Jedwali Na 6: Idadi ya vituo vya Afya vilivyofanyiwa utafiti..... 10
Jedwali Na 7: Idadi ya Akina mama wajawazito waliopima na kujifungua..... 11
Jedwali Na 8: Vifo vya watoto wachanga..... 12
Jedwali Na 9: Vifo vya watoto chini ya miaka 5 13
Jedwali Na 10: Vifo vya akina mama wajawazito..... 14
Jedwali Na 11: Uwiano wa Mwalimu kwa wanafunzi..... 15
Jedwali Na 12: Idadi ya wanafunzi kwa madaraja ya ufaulu kidato cha nne Wilaya ya Tarime 17
Jedwali Na. 13: Madaraja ya ufaulu katika mtihani wa kidato cha nne, 2014 Wilaya ya Morogoro vijijini 18
Jedwali Na 14: Vifo vya watoto wadogo chini ya mwaka 1 Wilaya ya Morogoro Vijijini 18
Jedwali Na 15: Vifo vya watoto wadogo chini ya mwaka 1 Wilaya ya Urambo 19
Jedwali Na 16: Vifo vya watoto wadogo chini ya mwaka 1 Wilaya ya Ukerewe..... 19
Jedwali Na 17: Vifo vya watoto wadogo chini ya mwaka 1 Wilaya ya Mtwara vijijini 19
Jedwali Na 18: Vifo vya watoto wadogo chini ya mwaka 1 Wilaya ya Misungwi..... 19
Jedwali Na 19: Vifo vya watoto wadogo chini ya mwaka 1 Wilaya ya Urambo 20
Jedwali Na 20: Vifo vya watoto wadogo chini ya mwaka 1 Wilaya ya Morogoro Vijijini 21
Jedwali Na 21: Vifo vya watoto wadogo chini ya mwaka 1 Wilaya ya Iramba..... 21
Jedwali Na 22: Vifo vya watoto wadogo chini ya mwaka 1 Wilaya ya Mtwara Vijijini 21

Orodha ya Grafu

Grafu Na 1: Uwiano wa Udahili, Jinsi ya Kike na kiume katika baadhi ya wilaya utafiti..... 4
Grafu Na 2: Umbali anaotembea Mwanafunzi kuelekea shuleni kwa Mwaka 2014..... 8

Orodha ya Picha

Picha 1: Shule ya Sekondari Lubu - Magu..... 7
Picha 2: Hali ya Miundombinu Mbalimbali katika shule za sekondari zilizofanyiwa tafiti 2015..... 7
Picha 3: Miundombinu inavyoendelea kuboreshwa..... 17
Picha 4: Choo cha bweni la wasichana..... 17
Picha 5: Maabara 17
Picha 6: Bweni la wasichana Msimbati Sekondari Mtwara Vijijini 2015..... 18
Picha 7: Nyumba ya Muuguzi: Kituo cha Afya Msimbati 20

Orodha ya Majedwali

Jedwali Na 1: Idadi ya shule zilizohusika 3
Jedwali Na 2: Linabainisha uwiano wa jinsi ya kike na kiume Katika shule za sekondari..... 4
Jedwali Na 4: Uwiano wa Walimu na wanafunzi; Mwaka 2014..... 6
Jedwali la 5: Umbali anaotembea Mtoto kwenda Shuleni 8
Jedwali 6: Idadi ya vituo vya Afya vilivyofanyiwa utafiti 11
Jedwali 7: Idadi ya Akina mama wajawazito waliopima na kujifungua 12
Jedwali 8: Vifo vya watoto wachanga 13
Jedwali 9: Vifo vya watoto chini ya miaka 5..... 14
Jedwali 10: Vifo vya akina mama wajawazito 15
Jedwali Na 11: Uwiano wa Mwalimu kwa wanafunzi..... 17
Jedwali Na 12: Idadi ya wanafunzi kwa madaraja ya ufaulu kidato cha nne Wilaya ya Tarime 20
Jedwali Na. 13: Madaraja ya ufaulu katika mtihani wa kidato cha nne, 2014 Wilaya ya Morogoro vijijini 20
Jedwali Na 14: Vifo vya watoto wadogo chini ya mwaka 1 Wilaya ya Morogoro Vijijini 22

Jedwali Na 15: Vifo vya watoto wadogo chini ya mwaka 1 Wilaya ya Urambo 22
Jedwali Na 16: Vifo vya watoto wadogo chini ya mwaka 1 Wilaya ya Ukerewe 22
Jedwali Na 17: Vifo vya watoto wadogo chini ya mwaka 1 Wilaya ya Mtwara vijijini 22
Jedwali Na 18: Vifo vya watoto wadogo chini ya mwaka 1 Wilaya ya Misungwi 22
Jedwali Na 19: Vifo vya watoto wadogo chini ya mwaka 1 Wilaya ya Urambo 23
Jedwali Na 20: Vifo vya watoto wadogo chini ya mwaka 1 Wilaya ya Morogoro Vijijini 23
Jedwali Na 21: Vifo vya watoto wadogo chini ya mwaka 1 Wilaya ya Iramba 23
Jedwali Na 22: Vifo vya watoto wadogo chini ya mwaka 1 Wilaya ya Mtwara Vijijini 23

Orodha ya Grafu

Grafu Na 1: Uwiano wa Udahili, Jinsi ya Kike na kiume katika baadhi ya wilaya utafiti..... 4
Grafu Na 2: Umbali anaotembea Mwanafunzi kuelekea shuleni kwa Mwaka 2014..... 9

Orodha ya Picha

Picha 1: Shule ya Sekondari Lubu - Magu..... 7
Picha 2: Hali ya Miundombinu Mbalimbali katika shule za sekondari zilizofanyiwa tafiti 2015..... 7
Picha 3: Miundombinu inavyoendelea kuboreshwa..... 17
Picha 4: Choo cha bweni la wasichana..... 17
Picha 5: Maabara 17
Picha 6: Bweni la wasichana Msimbati Sekondary Mtwara Vijijini 2015..... 18
Picha 7: Nyumba ya Muuguzi: Kituo cha Afya Msimbati 22

VIFUPISHO

TCDD	Tanzania Coalition on Debt and Development
MKUKUTA	Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania
MSD	Medical Stores Department
UN	United Nations
UKIMWI	Upungufu wa Kinga Mwilini
KM	Kilomita
UNICEF	The United Nations Children's Fund

HALI YA ELIMU NA AFYA NA CHANGAMOTO ZAKE NCHINI TANZANIA MWAKA 2014

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.0. Msingi wa mradi wa utafiti

Umaskini ni changamoto kubwa inayoikabili Tanzania na nchi nyingine nyingi zinazoendelea pamoja na taarifa zinazoashiria kuimarika na kukua kwa uchumi wa Tanzania kwa wastani wa asilimia 7, tangu mwaka 2005, sambamba na malengo ya MKUKUTA ya ukuaji wa asilimia 6-8 kwa mwaka. Sababu nyingi zimekuwa zikielezwa kupelekea hali hii ya umaskini hapa nchini ambazo ni pamoja na sera za uchumi: Sera za fedha na matumizi ya Serikali kutotosheleza kukuza uchumi unaonufaisha wengi, huduma zisizotosheleza katika sekta ya kilimo, uwekezaji usiotosheleza katika viwanda mijini na vijijini, teknolojia duni, mila potofu na desturi zisizo na tija katika kuleta maendeleo (ubaguzi wa kijinsia; ushirikina), kuwa na deni kubwa la Taifa nk.

Katika jitihada za kupunguza na kuondoa umaskini, Tanzania imeanzisha mikakati ya makusudi ambayo ni mwongozo wa maendeleo ya jamii na uchumi. Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inatamka kuwa Tanzania itakuwa imefuta umaskini ifikapo mwaka 2025 ambapo Tanzania itakuwa imefikia kiwango cha kati cha maendeleo. Katika kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Tanzania imetengeneza mkakati maalum wa muda ambao ni Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA II) 2010/2011 – 2014/2015 katika kufikia matarajio ya Dira ya Taifa na Malengo ya Milenia. Ili kutekeleza kikamilifu MKUKUTA II, sekta zinahusisha mipango yake kwa kuoanisha na malengo ya MKUKUTA II.

Lengo kuu la MKUKUTA ni kukuza uchumi na kuondoa umaskini kwa kutegemea nguzo kuu zifuatazo: amani, utulivu na umoja; utawala bora; jamii iliyoelimika na inayojifunza; uchumi imara; endelevu, usiotegemea sekta moja, nyumbulifu, wenye ushidani, na wenye kuleta maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii

Utekelezaji wa MKUKUTA II katika kuondoa umaskini na kukuza uchumi umejikita katika nguzo kuu tatu za kipaumbele, ambazo ni:kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato, ubora wa ustawi wa jamii na utawala bora na uwajibikaji.

1.1. Ushiriki wa Asasi za Kiraia katika Maendeleo

Ili kuhakikisha ufanisi na utekelezaji makini wa MKUKUTA II usimamizi ni suala muhimu hasa pale mpango huu unapojikita katika kuboresha maisha na ustawi wa jamii hasa kwa watu walio maskini zaidi pamoja na wale walio katika mazingira hatarishi.

Usimamizi mzuri ni pamoja na upatikanaji wa taarifa sahihi kwa muda mwafaka na ili kufanikisha upatikanaji wa taarifa sahihi kwa wakati, serikali kupitia mfumo wake wa kitaifa wa usimamiaji wa programu ya kupunguza umaskini, inahimiza usimamizi shirikishi wa asasi za kiraia. Katika muktadha huo, TCDD imejikita katika mradi wa kukusanya takwimu, taarifa na vielelezo vitakavyosaidia ufikwaji wa maamuzi na uimarishaji wa uwezo wa asasi zisizo za kiserikali ziweze kujihusisha kwa usahihi zaidi katika majadiliano ya kisera lakini pia kuangalia utekelezaji, ufuatiliaji, na tathmini ili kujiridhisha na ufanisi wa MKUKUTA II kwa jamii ya Tanzania kuelekea katika Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025

Malengo ya MKUKUTA II yanaweza kufikiwa endapo tu wadau mbalimbali wa maendeleo watashiriki kikamilifu katika utekelezaji wake. Wadau wa maendeleo si wale tu walio katika taasisi za kiserikali na Bunge, bali pia walio katika asasi za kijamii, sekta binafsi, wafadhili na jamii yote kwa ujumla. Wadau wanahimizwa kushiriki kikamilifu katika utekelezaji ili kujenga hamasa na hali ya umiliki wa mkakati huu kwa jamii.

1.2. Njia za Utafiti

Utafiti huu ulihusisha ukusanyaji wa taarifa kutoka kwa wadau mbalimbali wa elimu na afya juu ya utekelezaji wa Mpango wa MKUKUTA II katika wilaya 12 zilifanyiwa utafiti na kujionea hali halisi kwa kutazama kiwango cha utekelezaji wa miradi mbalimbali inayohusisha MKUKUTA II.

1.3. Sampuli

Sampuli iliyotumika katika utafiti huu zilipatikana kutokana na mapendekezo yaliyotokana na wadau na wanachama wa TCDD. Kila wilaya ilichagua shule kumi za sekondari na vituo vitano vya huduma ya afya katika wilaya husika.

1.4. Zana za ukusanyaji takwimu

Takwimu zilikusanywa kwa kutumia madodoso na majadiliano vikundini. Madodoso yalijumuisha maswali ya wazi na yasiyo ya wazi kwa wilaya zote. Madodoso hayo yalikuwa yamegawanyika katika sehemu kuu tatu nazo ni madodoso kwa wakuu wa shule za sekondari, na waganga wa vituo vya afya, na zahanati, madodoso kwa maafisa elimu wilaya na mganga mkuu wa kila wilaya husika na madodoso ya namna ya uendeshaji wa majadiliano kwa vikundi ambayo yaliendeshwa kwa kushirikisha kamati za afya na za shule katika ngazi mbalimbali za wilaya husika, wazazi na wanafunzi.

1.5. Baadhi ya mambo muhimu yaliyoangaliwa kwenye utafiti huu

Uwiano wa wanafunzi na vitabu (kiada), walimu, madarasa, madawati, miundombinu nk, ufaulu wa wanafunzi, taarifa kuhusu mfumo wa bajeti na ushirikishwaji wa walengwa, uwajibikaji wa jamii katika uandaaji, utekelezaji na usimamiaji wa bajeti katika maeneo yao, kutambua kama malengo ya MKUKUTA II katika sekta ya elimu na afya yamefikiwa, changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa MKUKUTA II katika wilaya husika hususan katika sekta ya elimu na afya na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa bajeti za shule na vituo vya afya.

SURA YA PILI

2.0. MATOKEO YA UTAFITI KATIKA SEKTA YA ELIMU

Elimu ni moja ya vipaumbele muhimu katika utekelezaji wa MKUKUTA II ikiwa ni nguzo mojawapo ya kuboresha maisha ya jamii kwa ujumla. Moja ya matarajio makubwa katika sekta hii ya elimu ni kuongeza uwezekano wa wananchi wengi kuwa na fursa ya kupata elimu bora katika ngazi mbalimbali, hasa katika elimu ya msingi na sekondari. Jumla ya wilaya 12 zilihusishwa katika utafiti huu ambazo ni Bunda, Biharamulo, Magu, Rugwe, Mufindi, Kishapu, Kigoma vijijini, Mkuranga, Manispaa ya Lindi, Bahi, Newala na Songea. Jumla ya shule za serikali 112 hasa shule za kata zilitarajiwa kuhusika katika utafiti huu, lengo likiwa ni kutembelea shule 10 za sekondari kutoka katika kila wilaya husika. Jedwali hapa chini linafafanua.

2.1. Wilaya na Idadi ya shule zilizohusika katika utafiti huu

Jedwali Na 1: Idadi ya shule zilizohusika

	Wilaya	Idadi ya Shule	Wilaya	Idadi ya Shule
1.	Bunda	10	Kigoma vijijini	10
2.	Rungwe	8	Lindi Manispaa	8
3.	Magu	10	Biharamulo	0
4.	Mufindi	10	Bahi	0
5.	Mkuranga	10	Newala	0
6.	Kishapu	10	Songea Vijijini	7

Chanzo: Utafiti 2015

Matokeo ya utafiti katika sekta hii ya elimu yamegawanywa katika maeneo muhimu kama yalivyoainishwa katika mwongozo wa utekelezaji wa MKUKUTA II yaani MKUKUTA II Monitoring Master Plan; Cluster II. Idadi ya wanafunzi wa shule za sekondari, uwiano wa walimu kwa wanafunzi, viwango vya ufaulu na idadi ya wanafunzi wanaoendelea na masomo ya juu/ufundi, mazingira safi na bora ya kujifunzia kwa wanafunzi (miundombinu shuleni), uwiano wa vitabu vya kiada na wanafunzi, utekelezaji wa bajeti katika sekta ya elimu, umbali anaotembea mtoto kwenda shule na uandikishaji wa wanafunzi wenye ulemavu.

2.2. Uwiano wa Udahili wa wanafunzi wa kike na kiume katika shule za sekondari

Sera ya Elimu ya mwaka 2014 inataka uwiano unaoendana wa uandikishaji wa wanafunzi wa jinsi ya kike na jinsi ya kiume katika ngazi mbalimbali za elimu. Katika ngazi ya elimu ya sekondari ni 1:09, lakini takwimu za utafiti uliofanywa na TCDD unaonesha kutokuwa na uwiano sawa kwa mujibu wa sera katika uandikishaji na kumekuwa na kushuka kwa ufaulu hasa kwa wanafunzi wa jinsi ya kike kwa kukatisha masomo yao hasa pale wanapokuwa wanavuka kutoka hatua moja ya kimasomo kwenda hatua nyingine.

Kuna baadhi ya wilaya kama vile Bunda, Lindi Mjini na Kigoma Vijijini udahili wa wanafunzi wa kiume ni mkubwa kuliko wa kike na wilaya za Mkuranga na Mufindi ambapo udahili wa wanafunzi wa kike ulikuwa ni mkubwa kuliko wa wanafunzi wa kiume.

Kuna sababu mbalimbali ambazo zinatajwa kukwamisha zoezi la udahili wa wanafunzi kidato cha kwanza na kuongezeka kwa uwiano wa wanafunzi wa kike na kiume. Sababu hizo ni:-

- Mimba kwa wanafunzi wa kike
- Hali ngumu ya maisha kwa wazazi
- Mwamko duni wa wazazi juu ya umuhimu wa elimu.

Jedwali Na 2: Uwiano wa jinsi ya kike na kiume katika shule za sekondari

Wilaya	Bunda		Mkuranga		Mufindi		Kigoma(V)		Kishapu	
Mwaka 2014	Me	Ke	Me	Ke	Me	Ke	Me	Ke	Me	Ke
	699	418	989	1150	582	669	540	277	0	0

Chanzo: Utafiti 2015

Pia katika ngazi ya wilaya, udahili umeongezeka japokuwa umetofautiana kutoka jinsi moja na nyingine kutokana na hali ya mwamko wa elimu katika wilaya husiku na changamoto zingine. Kama ilivyobainishwa katika wilaya zingine hapo juu, Wilaya ya Rungwe kwa mwaka 2014 wanafunzi wa kiume waliodahiliwa walikuwa 1424 na wanafunzi wa kike walikuwa 1652. Na wanafunzi 128 hawakuripoti kwa sababu ya: utoro, kudahiliwa shule binafsi na wanafunzi 16 kupata mimba. Katika Wilaya ya Lindi (Mjini) wanafunzi 1756 wakiume walidahiliwa na wanafunzi 1230 wa jinsi ya kike walidahiliwa. Na katika wilaya ya Kishapu utafiti unaonesha kuwa wanafunzi walioshindwa kuripoti katika shule walizopangiwa; wavulana walikuwa 258 na wasichana walikuwa 245.

Grafu Na 1: Uwiano wa Udahili, Jinsi ya Kike na kiume katika baadhi ya wilaya utafiti



Chanzo: Utafiti 2015

Pia utafiti unaonesha kuwa baadhi ya shule kama vile Chikonji Sekondari kutoka katika Manispaa ya Lindi ina idadi ndogo sana ya wanafunzi ambapo kwa shule nzima kuanzia kidato cha I hadi cha IV kuna wanafunzi 110 na kati ya hao ni wanafunzi 47 tu ni wa jinsi ya kike.

Maoni: Juhudi za makusudi zinatakiwa kuchukuliwa ili kuongeza udahili wa wanafunzi hasa wa jinsi ya kike lakini pia elimu itolewe kwa wazazi ili kuongeza hamasa na waweze kuwapeleka kwa wingi watoto wao shule na hii pia itasaidia kuwaepusha watoto na mimba za utotoni.

2.3. Kiwango cha ufaulu mtihani kidato cha nne na waliojiunga kidato cha tano

Utafiti unaonyesha kuwa hali ya ufaulu wa wanafunzi kwa shule za sekondari sio mzuri kwa mwaka 2014 hasa kwa wanafunzi wa jinsi ya kike ambao umekuwa chini zaidi ukilinganisha na wanafunzi wa jinsi ya kiume. Jedwali hapo chini linafafanua.

Jedwali Na 3: Ufaulu wa wanafunzi Mwaka 2014

WILAYA	MADARAJA											
	I			II			III			IV		
	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla
Bunda	3	0	3	18	2	20	44	7	51	74	53	127
Rungwe	0	0	33	0	0	291	0	0	626	0	0	1241
Kishapu	6	0	6	73	5	78	147	31	178	247	144	391
Kigoma	0	0	1	0	0	3	0	0	65	0	0	204
Lindi	th	th	th	th	th	th	Th	th	th	th	th	th
Mkuranga	0	0	2	0	0	15	0	0	35	0	0	162

Chanzo: Utafiti 2015

Kama ilivyo kwa wilaya zingine, katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda hali ya ufaulu kwa wanafunzi wa jinsi ya kike umekuwa chini sana, mfano kwa shule 10 zilizofanyiwa utafiti ni wanafunzi 3 tu ambao ni wa jinsi ya kiume ndiyo waliopata daraja la kwanza, daraja la II ni wanafunzi 20 ambapo wanafunzi wa jinsi ya kiume walikuwa 18 na wa jinsi ya kike ni wanafunzi 2 tu. Daraja la III walikuwa 51, wanafunzi 44 ni wa jinsi ya kiume na wanafunzi 7 tu ni wa jinsi ya kike. Pia kwa shule zilizofanyiwa utafiti katika Wilaya ya Kishapu utafiti unaonesha ufaulu wa chini sana kwa wanafunzi wa jinsi ya kike kuliko wa jinsi ya kiume. Mfano ufaulu kwa daraja la I ulikuwa wanafunzi 6 ambao ni wa jinsi ya kiume tu na jinsi ya kike ni 0, daraja la II wanafunzi 78 ambapo wanafunzi wa jinsi ya kiume walikuwa 73 na jinsi ya kike ni 5 tu na daraja la III jumla walikuwa 178 ambapo jinsi ya kiume walikuwa 147 na jinsi ya kike walikuwa 31.

Pamoja na taarifa hapo juu, utafiti unaonesha kuongezeka kwa wanafunzi wanaopata ufaulu wa daraja 0. Mfano katika Wilaya ya Rungwe kwa mwaka 2014 ni wanafunzo 679 wamepata ufaulu wa daraja 0 sawasawa na 24% ya watahiniwa wote. Pia katika Wilaya ya Kishapu ni wanafunzi 201 waliopata ufaulu wa Daraja 0, jinsi ya kiume wanafunzi 118 na kike 83. Na Wilaya ya Mkuranga ni wanafunzi 118 kwa shule zilizofanyiwa utafiti sawa na asilimia 33% ya wanafunzi wote waliofanya mtihani huo.

2.4. Uwiano wa Walimu kwa Wanafunzi

Lengo la serikali ni kufikia uwiano wa 1:35 yaani mwalimu mmoja kwa wanafunzi 35 na lengo la MKUKUTA ni kufikia 1:25 katika darasa kwa shule za sekondari kuanzia kidato cha I hadi kidato cha 6. Kigezo hiki ni muhimu sana katika kutambua ubora wa elimu inayotolewa kwa kuzingatia kwamba usikivu wa wanafunzi darasani ni eneo muhimu sana ambalo linabidi lipewe kipaumbele, hasa kwa kuzingatia kwamba kwa kiwango kikubwa unaweza kuathiri ushiriki wa mwanafunzi katika masomo yake. Takwimu za utafiti huu zinaonesha kuwa bado kuna hitaji kubwa la walimu katika shule za sekondari, mfano:

Jedwali Na 4: Uwiano wa Walimu na wanafunzi; Mwaka 2014

Wilaya	2014	Wilaya	2014
Rungwe	1:21	Bunda	1:30
Kishapu	1:39	Lindi Manispaa	1:12
Mkuranga	1:36	Kigoma vijijini	1:40
Magu	1:54	Songea Vijijini	1:23
Mufindi	1:29	Biharamulo	TH



Chanzo: Utafiti 2015

Lengo la MKUKUTA II ni kufikia mwaka 2015, shule za sekondari zinafikia uwiano wa 1:25 yaani mwalimu mmoja kwa wanafunzi 25 katika darasa. Uwiano sahihi kati ya mwalimu na wanafunzi katika darasa unamsaidia mwalimu kulimudu darasa lake na kutambua uwezo wa kila mwanafunzi na kuona namna ya kumsaidia katika masomo yao. Shule nyingi zilizofanyiwa utafiti zimeshindwa kufikia uwiano tarajiwa wa MKUKUTA II pamoja na ule wa sera ya elimu. Hivyo juhudi za makusudi zinatakiwa kuchukuliwa na serikali ili kufikia lengo la MKUKUTA II la uwiano wa 1:25 lakini pia kufikia lengo la sera ya elimu ya uwiano wa 1:35 na kuboresha elimu itolewayo hapa Tanzania

2.5. Hali ya Miundombinu Mashuleni

MKUKUTA II ilidhamiria kuboresha hali ya miundombinu katika shule za sekondari, hii ni pamoja na kuwa na maji ya kutosha, mazingira safi, mabweni ya wasichana, umeme nk, mazingira yatakayowazesha wanafunzi wa jinsi ya kike kuendelea vizuri na masomo pasipo kuathiriwa na mabadiliko yatokanayo na mabadiliko ya miili yao.

Utafiti unabainisha kuwa, hali ya miundombinu katika shule nyingi sio ya kuridhisha hivyo kupelekea kuathiri maendeleo ya wanafunzi kitaaluma. Uwepo wa maji safi, vyoo na mabweni ni muhimu sana kwani upungufu au kutokuwepo kwa miundombinu hiyo hupelekea wanafunzi wengine kuacha shule na wengine kupata mimba wakiwa masomoni.

Mfano: Kati ya shule 10 zilizofanyiwa utafiti katika **Wilaya ya Bunda** ni shule 2 tu ndizo zenye na mabweni kwa ajili ya wanafunzi wa kike. Katika shule hizo kumi ni shule 3 tu ndizo ambazo maabara zake zimekamilika (yaani kuna jengo, vifaa na walimu husika).

Pia katika **Wilaya ya Rungwe**, kati ya shule tisa (9) zilizofanyiwa utafiti ni shule moja tu (1) ambayo ni shule ya kutwa ya Rungwe Sekondari yenye bweni kwaajili ya wanafunzi wa jinsi ya kike na shule zingine 8 hazina mabweni.

Katika **Wilaya ya Magu** kati ya shule 10 zilizofanyiwa utafiti ni shule tatu (3) ndizo zenye maabara na zingine hazina; na uwiano wa matundu ya vyoo kwa wanafunzi ni 1:46 ambao ni mkubwa kwa mujibu wa sera. Mfano katika shule ya Sekondari Lubugu, Wilaya ya Magu imekutwa na idadi ya wanafunzi 655 kwa mwaka 2015 na ikiwa na matundu ya vyoo 8 tu (kwa uwiano sawa wa jinsi ya kike na kiume); hii ni sawa na uwiano 1:81; yaani tundu moja la choo hutumiwa na wanafunzi 81 katika shule hiyo. Sera inaelekeza kuwa tundu moja la choo wanafunzi 25 yaani (1:25) kwa wanafunzi wa jinsi ya kike na 1:30 kwa wanafunzi wa jinsi kiume.

Utafiti unaonesha kuwa ushiriki wa wananchi katika ujenzi wa maabara na mabweni ya wanafunzi umekuwa wa kulazimishwa badala ya wananchi kujitolea wao wenyewe kwa kuhamasishwa juu ya umuhimu wa uwepo wa miundombinu hiyo ili waweze kuona kuwa miundombinu hiyo ni ya kwao ili washiriki katika utunzaji na ukarabati.

Picha Na 1: Shule ya Sekondari Lubu:Magu; wakati na Baada ya TCDD kufanya ufuatiliaji Shuleni hapo

Wakati wa ufuatiliaji (2014) **Baada ya Ufuatiliaji (2015)**

Picha 2: Hali ya Miundombinu Mbalimbali katika shule za sekondari zilizofanyiwa tafiti 2015

Utafiti 2015: Maabara Bugamba Sekondari, Kigoma Vijijini

Maabara Kinyanambo Sekondari: Mufindi

Ihongole Sekondari: Mufindi

Utafiti 2015: Choo wa Wavulana 247: Ngwamabanza Sekondari: Magu

Upungufu na ucheleweshaji wa fedha zilizotengwa katika bajeti, hamasa ndogo kutoka kwa wazazi kumechangia sana miundombinu mingi kuwa katika hali mbaya na isiyo ridhisha hivyo kuathili maendeleo ya taaluma katika shule nyingi zilizotembelewa.

2.6. Umbali anaotembea mtoto kwenda shule mwaka 2015

Utafiti huu pia ulijikita katika kubaini umbali anaotembea mwanafunzi kutoka makazi wanakoishi kuelekea shuleni, hii ni baada ya kujiridhisha kwamba umbali mrefu anaotembea mwanafunzi kuelekea shuleni umekuwa na athari kubwa katika maendeleo ya taaluma ya mwanafunzi husika. Mwanafunzi hufika shuleni akiwa amechoka kutokana na kutembea umbali mrefu, wanafunzi wengine huacha masomo na ni rahisi kwa watoto wa kike kupata mimba. Utafiti huu umebaini hali ifuatayo:-

Jedwali la 5: Umbali anaotembea mtoto kwenda shuleni

WILAYA	UMBALI KWA SIKU(KM)	UMBALI KWA WIKI(KM)
Bunda	6	30
Biharamulo	6	30
Magu	8	40
Rungwe	7	35
Mufindi	6	30
Kishapu	8	40
Kigoma vijijini	0	0
Lindi Manispaa	5	25
Mkuranga	5	25
Bahi	3	15
Newala	28	140
Songea	7	35

Chanzo: Utafiti 2015

Grafu Na 2: Umbali anaotembea Mwanafunzi kuelekea shuleni Kwa Mwaka 2014



Chanzo: Utafiti 2015

2.7. Mafanikio

Kuna mafanikio yaliyoweza kubainishwa katika maeneo mbalimbali katika sekta ya elimu kama vile ujenzi wa madarasa mapya, uboreshwaji wa miundombinu ya vyoo na maabara umeongezeka japokuwa katika maabara nyingi zilizojengwa yamekuwa ni majengo tu bila vifaa na walimu. Vitabu vya kujifunzia vimeongezeka, bajeti kwaajili ya maendeleo ya elimu imeongezeka na idadi ya wanafunzi shule za sekondari imeongezeka.

2.8. Changamoto

Fedha zinazotengwa kwaajili ya maendeleo ya elimu hazitoshi lakini pia hazifiki kwa wakati, kukosekana kwa takwimu muhimu katika shule mbalimbali, ukosefu wa samani muhimu za shule; kama vile viti, meza, madawati. Kwa mwaka 2015 kulikuwa na changamoto ya wakuu wa shule na baadhi ya wadau kukataa kutoa maoni kutokana na kuhusisha zoezi hilo na siasa za vyama vya upinzani. Wakuu wa shule kutokuwa tayari kutoa taarifa zinazohusu maendeleo ya shule, ukosefu wa mabweni na umbali mrefu kutoka nyumbani kwenda shule na wazazi kutowajibika ipasavyo kwa watoto wao kimaadili.

2.9. Mapendekezo

Tunapendekeza bajeti ya elimu iongezwe ili kuboresha miundombinu ya shule na wafanyakazi, ujenzi wa maabara na vifaa vyake, mabweni, na madarasa. Wazazi wawajibike kwaajili ya maendeleo ya kitaaluma ya wanafunzi, wazazi washirikiane na serikali kuanzia katika ngazi ya serikali ya mtaa katika kuboresha miundombinu ya shule; na wadau wa elimu wanapaswa kuisimamia serikali ipasavyo katika kutekeleza malengo ya MKUKUTA II kabla ya awamu hii kumalizika mwaka 2015.

SURA YA TATU

3.0. MATOKEO YA UTAFITI KATIKA SEKTA YA AFYA

Kama ilivyo kwa eekta ya elimu, sekta ya afya pia ni muhimu sana katika kujihakikishia taifa la watu wenye afya. Jamii yenye afya njema na ustawi mzuri ni muhimu sana katika kuongeza uzalishaji kwa ngazi zote yaani katika ngazi ya familia na katika ngazi ya Taifa kwa ujumla. Taifa lolote lenye nguvu kiuchumi na kisiasa na kimaendeleo hujengwa na jamii yenye afya njema. Kama ilivyo katika sekta ya elimu, sekta ya afya imepewa kipaumbele chini ya mpango wa MKUKUTA II ambapo utekelezaji wake umeongeza juhudi za serikali katika sekta ya afya na kuleta matokeo chanya hasa katika bajeti na mambo mengine kwa ujumla. Katika sekta ya afya MKUKUTA II umejikita katika; *kudhibiti vifo vya watoto wachanga wakati wa kujifungua, kupunguza vifo vya watoto chini ya miaka mitano*, *idadi ya kinamama wanaojifungulia katika vituo vya afya*, *kuboresha lishe kwa watoto*, *vifo vya akinamama wakati wa kujifungua na upatikanaji wa maji safi na salama mijini na vijijini.*

Takwimu mbalimbali za ufanisi wa bajeti ya serikali kwaajili ya mkakati wa kupunguza umaskini MKUKUTA II katika sekta ya afya zilikusanywa katika ngazi ya wilaya. Jumla ya wilaya kumi na mbili (12) zilihusishwa katika utafiti huu. Jumla ya vituo vya afya na zahanati 62 zilihusika kama jedwali linavyothibitisha.

Jedwali 6: Idadi ya vituo vya Afya vilivyofanyiwa utafiti

WILAYA	VITUO VYA AFYA
Bunda	5
Rungwe	7
Mufindi	5
Kishapu	6
Kigoma	4
Lindi	5
Mkuranga	7
Bahi	5
Newala	5
Songea	0
Magu	5

Chanzo: Utafiti 2015

3.1. Hali ya afya kutokana na utafiti uliofanywa kwenye wilaya

Jedwali 7: Idadi ya Akina mama wajawazito waliopima na kujifungua

Wilaya	Waliopima	Waliojifungua	Asilimia
Bunda	1618	867	53%
Rungwe	82	57	70%
Mufindi	1021	550	43%
Mkuranga	9124	8083	88%
Kigoma Vijijini	2022	865	65%
Lindi Manispaa	1558	646	41%



Chanzo: Utafiti 2015

Idadi ya akinamama wajawazito wanaohudhuria kliniki imeongezeka kwa kiwango kikubwa. Pamoja na ongezeko hilo; **Utafiti 2015** unabainisha kuwa bado kuna idadi kubwa ya akinamama wajawazito kutohudhuria vituo vya afya au zahanati wakati wa kujifungua kama inavyoonekana hapo juu kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo:-

i). Baadhi ya wanawake kujifungualia nyumbani
ii). Wengi kwenda kujifungulia katika hospitari za wilaya ambako hudumu za kiafya ni nzuri
iii). Wengine taarifa zao kutopatikana katika vituo walivyohudhuria kliniki na kujifungulia.

Elimu ya uzazi salama inatakiwa kwa kiasi kikubwa katika maeneo mbalimbali, hii itawezesha kuleta muamko kwa akinamama wajawazito kuhudhuria kliniki wakati wa ujauzito na wakati wa kujifungua kwaajili ya afya ya mama na mtoto. Lakini pia serikali inajukumu la kuboresha miundombinu na vifaa tiba katika zahanati na vituo vya afya ili mazingira ya akinamama kujifungulia yawe salama.

3.2. Vifo vya watoto wachanga (infanty mortality rate)

Utafiti unaonesha kuwa idadi ya vifo vya watoto chini ya mwaka mmoja na wale wasiotimiza siku 28 baada ya kuzaliwa kuwa ni kubwa kuliko kawaida na idadi hiyo ya vifo inaonekana kuongezeka badala ya kupungua. Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali na wananchi iboreshe miundombinu ili kuwawezesha wanawake wajawazito na watoto wachanga kufikiwa na kutumia huduma za afya ili kunusuru vifo vya watoto hawa.

Jedwali 8: Vifo vya watoto wachanga

Wilaya	2013	2014	Jumla
Mkuranga	79	99	247
Magu	96	50	510
Lindi	20	30	50
Bahi	3	2	*5
Mufindi	0	97	97



Chanzo: Utafiti 2015

Lengo la MKUKUTA II ni kupunguza uwiano wa vifo vya watoto wachanga (Infant Mortality rate) kutoka vifo 51 kwa watoto 1000 waliozaliwa hai yaani (51/1000) katika mwaka 2009/2010 hadi kufikia vifo 38/1000 kufikia mwaka 2015.

Kwa mujibu wa Benki ya Dunia hapa Tanzania, vifo vya watoto wachanga (Per 1000 livebirths) kwa mwaka 2015 imefikia 35/1000 (live births). Taarifa hizi zinaonesha kuvuka lengo lililowekwa na MKUKUTA II la 38/1000. Taarifa za utafiti huu, bado zinaonesha tatizo kuwa sugu na vifo kuongezeka kwenye baadhi ya maeneo hii ni kutokana na changamoto mbalimbali za vifaa tiba kuwa duni lakini pia magonjwa kama vile:-

- Severe birth asphyxia
- Intrauterine fetal death (IUFD) secondary to maternal infection
- Neonatal infection
- Prematurity
- Hypoglycaemia

Sababu zingine zikiwemo ukosefu wa vituo vinavyotoa huduma za afya hasa vijijini, ukosefu wa vifaa tiba muhimu, uhaba wa wataalamu wa afya, umbali kuvifikia vituo vya afya, kujifungulia nyumbani, umaskini, kuugua malaria hasa kwa watoto.

3.3. Vifo vya Watoto chini ya Miaka 5 (underfive mortality rate)

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia MKUKUTA II imekusudia kupunguza vifo vya watoto chini ya miaka 5 kutoka 81 kwa 1000 yaani (81/1000) mwaka 2009/2010 hadi 54 kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa hai (54/1000) kufikia mwaka 2015.

Utafiti uliofanywa na TCDD 2015, unabainisha kuendelea kuwepo kwa tatizo hilo japokuwa taarifa za Benki ya Dunia kwa mwaka 2014 ni kwamba: Tanzania imeweza kupunguza vifo hivyo hadi kufikia kiwango cha watoto 50 kati ya 1000 walio hai yaani (50/1000), maana yake ni kwamba imevuka matarajio yaliyopangwa kufikiwa na MKUKUTA II ifikapo 2015.

Hoja ya msingi ni kwamba serikali ihakikishe kwamba huduma muhimu kwa watoto chini ya miaka 5 inapatikana na inatolewa kama vile chanjo muhimu ili kuwakinga watoto na magonjwa mfano: (*vaccine against diphtheria, pertussis (whooping cough), tetanus and hepatitis B* zinatolewa siku ya kuzaliwa na baada ya kuzaliwa. Maeneo mengi ya vijijini ndiyo yanaathirika zaidi na vifo kutokana na huduma muhimu za kiafya kutokufika.

Jedwali 9: Vifo vya watoto chini ya Miaka 5

Wilaya	2013	2014	Jumla
Mkuranga	108	127	235
Magu	92	85	177
Lindi Manispaa	*4	63	67
Bahi	TH	TH	TH
Mufindi	TH	58	58



Chanzo: Utafiti 2015

3.4. Vifo vya akina mama wajawazito wakati na baada ya kujifungua (maternal mortality rate)

Lengo ni kubaini ni kwa kiwango gani tatizo hili limekuwa kubwa katika maeneo yaliyofanyiwa tafiti. Kuna changamoto mbalimbali ambazo zimebainika wakati wa kukusanya taarifa za vifo vya akina mama wajawazito, miongoni mwa changamoto hizo ni kukosekana kwa taarifa muhimu juu ya tatizo hili; sio kwamba vifo havitokei la hasha, bali namna ya uhifadhi wa kumbukumbu umekuwa ni tatizo na madaktari viongozi wa vituo mbalimbali vilivyotembelewa wamekili kuwepo kwa tatizo hili.

Tatizo bado ni kubwa, hii ni kwa mujibu wa utafiti uliofanywa 2015: Ilitarajiwa kwamba vifo vya akina mama wajawazito kushuka kutoka vifo 454 kwa 100,000 walio hai mwaka 2011 hadi kufikia 382/100,000 kwa mwaka 2015 pale ambapo serikali itajidhatiti kwa kufanya uwekezaji mkubwa kwa vifaa tiba na wataalamu wa kutosha hasa maeneo ya vijiji.

Hivi sasa kati ya wanawake 3/1000 wa vijijini wenye umri wa kuzaa (15-49) wapo katika hatari ya kufa wakati wa kujifungua au baada ya kujifungua na wanawake 2/1000 katika maeneo ya mjini wapo katika hatari hiyo ya kufa hii ni kwa mujibu wa; Mortality and Health Report (2015); National Bureau of Statistics, Wizara ya Fedha – Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Hata hivyo vifo vya akina mama wajawazito kwa maeneo ya mijini ni kubwa zaidi kwa uwiano wa 443/100,000 kuliko maeneo ya vijijini kwa uwiano wa 336/100,000.

Hali ya vifo vya mama wajawazito bado ni kubwa pamoja na mkakati uliowekwa na MKUKUTA II ili kupunguza tatizo hilo. Hivi sasa, vifo vya akina mama wajawazito kwa Tanzania vinakadiliwa kuwa 435/100,000 kwa kila wamama walio hai. Hivyo basi juhudi za makusudi zinatakiwa na serikali yenye dhamana pamoja na mikakati endelevu ili kupunguza tatizo hilo katika nchi yetu

Jedwali 10: Vifo vya akina mama wajawazito

Wilaya	2014	Jumla
Mkuranga	6	6
Magu	20	20
Lindi Manispaa	*4	4
Bahi	0	0
Mufindi	10	10
Bunda	*4	4



Chanzo: Utafiti 2015

3.5. Changamoto

Uhaba wa wataalamu wa afya kama vile madaktari, matabibu, wauguzi na wakunga, ufinyu wa bajeti, na vifaa tiba vimekuwa ni changamoto katika maeneo mengi ya za afya. Vifo vya mama na mtoto bado ni changamoto, mazingira ya ushirikina katika baadhi ya vituo na kufanya baadhi ya wahudumu wa afya kushindwa kuishi katika nyumba zao na baadhi ya viongozi hufanya kazi kimazoea.

3.6. Mapendekezo

Ili kuboresha huduma za afya bajeti katika sekta hii inahitajika kuongezwa zaidi, bajeti tengwa ya afya ifike kwa wakati ili ziweze kufanya kazi kwa wakati, elimu ya afya kwa jamii iimarishwe, miundombinu ya afya iongezwe na kuboreshwa na wafanyakazi waongezwe na baadhi ya watendaji wanatakiwa kubadilishwa vituo vya kazi ili kuepuka kufanya kazi kwa mazoea.

SEHEMU YA NNE

UFUATILIAJI WA MRADI WA 2011-2014

4.0. UTANGULIZI

Sehemu hii inahusisha taarifa za mradi uliotekelezwa na TCDD kwa kipindi cha mwaka 2011 hadi 2014 katika kufuatilia umaskini kupitia MKUKUTA II katika sekta za elimu na afya. Katika hatua hii taarifa zinazokuja zinajaribu kuonyesha matokeo ambayo mradi imeyaleta baada ya utekelezaji wa mradi kukamilika eneo husika.

4.1. SEKTA YA ELIMU

Sehemu hii ni ufupisho wa ufuatiliaji wa sekta ya elimu uliofanyika mwaka 2015 kwa mwaka 2014.

4.2. Uwiano wa ddadi ya walimu kwa wanafunzi

Lengo ni kuangalia kama ongezeko la walimu katika shule sambamba na ongezeko la wanafunzi katika shule zilizotembelewa katika utafiti huu. Hii itapimwa na sera inayotuongoza kuwa uwiano unaotakiwa kati ya walimu na wanafunzi ni 1:35. Hii inasaidia kupima kiwango na ubora wa elimu itolewayo kwa wanafunzi husika. Uwiano mzuri kati ya walimu na wanafunzi kunamuwezesha mwalimu kulimudu darasa lake vizuri lakini kumuelewa kila mwanafunzi na hitaji lake la msingi; Jedwali linaonesha.

Jedwali Na 11: Uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi

Wilaya	2014	Wastani
Kilolo	1:25	1:25
Iramba	1:26	1:26
Mtwara	1:47	1:47
Misungwi	1:65	1:65
Tarime	1:43	1:43
Urambo	1:33	1:33
Morogoro	1:34	1:34

Chanzo: Taarifa za ufuatiliaji 2015

Hali ya uwiano wa walimu kwa wanafunzi katika shule zilizotembelewa umezidi kuimarika, hii ni kutokana na serikali kuendelea kuajili walimu. Utafiti unaonesha, Wilaya ya Mtwara, Misungwi na Tarime ndizo ambazo wastani wake unaonesha kuwa juu kuliko ule wa serikali 1:35. Bado tunaendelea kuishauri serikali kuendelea kuajili walimu wengi zaidi hasa kwa mikoa iliyoko pembezoni na katika shule za kata.

4.3. Miundombinu ya Shule imeboreshwa

TCDD na mradi wa ufuatiliaji umewezesha miundombinu mingi katika shule za sekondari katika wilaya ambazo mradi huu umetekelezwa. Miundombinu mbalimbali yakiwemo madarasa, vyoo, mabweni, majiko nk yamezidi kuimarishwa siku hadi siku.

Picha Na 3: Miundombinu inavyoendelea kuboreshwa

Shule ya Sekendari Mahurunga: Mtwara 2015
Ujenzi unaendelea…..

Darasa Shule ya sekondari Rebu: Tarime 2015

Maabara Shule ya Sekondari Kinambeu: Iramba
Kwa ndani

Maabara Shule ya Sekondari Kinambeu:
Kwa nje

Pamoja na Uboreshwaji huo unaoendelea kufanywa na serikali, bado kuna changamoto kubwa ambazo zinahitajika kutatuliwa ili kuboresha miundombinu hiyo: **Mfano:**

Picha Na 4: Choo cha bweni la wasichana

Choo cha Bweni la wasichana:
Shule ya Sekondari Msimbati: Mtwara, 2015

Picha Na. 5: Maabara

Maabara na uhifadhi wa vifaa vyake
Tarime: 2015

Uwiano mkubwa kati ya tundu la choo na idadi ya wanafunzi wanapaswa kutumia choo hicho kwa mujibu wa sera na vingine havina milango na vingine ni vya muda mrefu hivyo vinashindwa kuwapa hifadhi na faragha wanafunzi hasa wa jinsi ya kike. Baadhi ya shule hazina maji na sio salama kiafya kwa yale yaliyopo, shule hazina umeme na hazivutii watoto kuendelea kusoma na kupelekea utoro kuongezeka.

Shule nyingi zilizotembelewa katika utafiti huu zimakutwa kuwa na *majengo ya maabara* (yasiyokuwa na vifaa na walimu wa taaluma hiyo). Pia shule kukosa mabweni ya wanafunzi wa jinsi ya kike ni tatizo: mfano; kati ya shule saba (7) zilizotembelewa Mtwara vijijini ni shule moja tu ya Msimbati yenye bweni la kike ambalo haliko kwenye hali nzuri na halitoshelezi.**Tazama Picha hapo chini:**

Picha Na 6: Bweni la Wasichana Msimbati Sekondari – Mtwara Vijijini 2015

Elimu bora bila miundombinu yenye tija haiwezekani, miundombinu michakavu au mibovu huwakatisha tamaa wanafunzi kuishi maisha ya bweni na wakati mwingine hupelekea wanafunzi kukatisha masomo yao.

4.4. Idadi ya Wanafunzi kwa Madaraja ya ufaulu katika mtihani wa Kidato cha Nne

Hali ya ufaulu katika mtihani wa kidato cha nne (4) si cha kuridhisha. Hali ya ufaulu imezidi kushuka pamoja na kuwa hali ya miundombinu inazidi kuimarika kutokana na uwekezaji unaofanywa na serikali kwa kushirikiana na wananchi. Ni matamanio ya kila mdau kuona hali ya miundombinu inaimarika sambamba na hali ya ufaulu kuongezeka.

Jedwali Na 12: Idadi ya wanafunzi kwa madaraja ya ufaulu kidato cha nne Wilaya ya Tarime

Mwaka		2014		
	DARAJA	Me	Ke	JUMLA
	1	1	0	1
	11	28	3	31
	III	58	23	81
	1V	141	95	236
	0	111	58	169
	Jumla	339	179	518



Chanzo cha utafiti: 2015

Jedwali Na 13: Madaraja ya ufaulu katika mtihani wa Kidato cha Nne, 2014 W/Morogoro Vijijini

Mwaka	2014							
Kata	Gwata		Mikese		Mkambarani		Kiloka	
Jinsi	Me	Ke	Me	Ke	Me	Ke	Me	Ke
Daraja la I	00	00	01	02	00	00	03	03
Daraja la II	01	04	01	05	00	00	06	04
Daraja la III	02	05	10	07	03	05	10	09
Daraja la IV	18	10	30	40	16	20	30	25
Jumla								

Chanzo cha utafiti: 2015

Utafiti unaonesha kuwa katika shule ya Mkambarani hapakuwa na ufaulu wa daraja la I na daraja la II. Waliofaulu kwa ushindi wa daraja la III walikuwa 08 na daraja la IV walikuwa 36, utafiti unaonesha kuwa wanafunzi 71 walipata daraja 0. Katika shule ya sekondari Mikese daraja la I walikuwa wanafunzi 03, daraja la II walikuwa wanafunzi 06, daraja la III wakiwa 17 na daraja la IV wakiwa 70 huku daraja 0 wakiwa wanafunzi 80. Utafiti pia unaonesha kata ya Kiloka ufaulu wa daraja I 05, daraja la II 10, daraja III wakiwa 19, daraja la IV 55 na daraja la 0 wakiwa wanafunzi 70. Vilevile Gwata hapakuwa na ufaulu wa daraja la I, huku kukiwa na wanafunzi 05 waliopata daraja la II, daraja la III wanafunzi 7 na daraja la IV 28 huku wanafunzi 34 wakipata daraja la 0.
Hii ndiyo hali halisi ya ufaulu katika shule nyingi hasa za kata zilizofanyiwa utafiti na TCDD kwa mwaka 2014. Ufaulu wa wanafunzi kwa madaraja ya juu umekuwa na wanafunzi wachache sana ukilinganisha na ufaulu wa madaraja ya chini.

4.5. Mapendekezo ya TCDD

Bado tunaendelea kuisihi serikali kuendelea kuwekeza kwenye elimu hasa kwa kuajiri walimu wa kutosha na maslahi yao yakiwa yameboreshwa. Imebainika kuwa kutokana na maslahi ya walimu wengi kuwa duni baadhi ya walimu wameamua kujikita katika biashara ya bodaboda ili kujiingizia kipato badala ya kuelekeza nguvu za katika kufundisha wanafunzi. Miundombinu kama vile maabara, madarasa, vyoo, mabweni, maji, umeme ni muhimu ikaboreshwa ili kutengeneza mazingira safi ya utolewaji wa elimu bora na sio bora elimu.

5.0. SEKTA YA AFYA KATIKA WILAYA

Ufuatao ni ufupisho wa ufuatiliaji wa sekta ya afya uliofanyika mwaka 2015 kwa ajili ya mwaka wa 2014.

5.1. Vifo vya watoto wadogo chini ya mwaka 1

Serikali kupitia mpango wa MKUKUTA II imekusudia kupunguza vifo vya watoto chini ya miaka 5 kutoka vifo 51 kwa watoto 1000 waliozaliwa hai yaani (51/1000) katika mwaka 2009/2010 hadi kufikia vifo 38/1000 kufikia mwaka 2015. Je hali halisi ipoje katika ngazi ya Halmashauri zetu?

Jedwali Na 14: Vifo vya watoto wadogo chini ya mwaka 1 Wilaya ya Morogoro Vijijini

Mwaka	2014				
Kata	Mikese	Gwata	Kiloka	Mkambalani	Wilaya
Chini ya Mwaka 1	00	00	00	00	123
Jumla	00	00	00	00	123

Chanzo: Utafiti 2015

Jedwali Na 15: Vifo vya watoto wadogo chini ya mwaka 1 Wilaya ya Urambo

	Kituo	Me	Ke
1.	Urambo Hospitali	16	17
2.	Uyumbu Zahanati	4	5
3.	Itundu Zahanati	2	7
4.	Usisya Zahanati	3	1
5.	Mungano Zahanati	1	5
	JUMLA	**26**	**35**

Chanzo: Utafiti 2015

Jedwali Na 16: Vifo vya watoto wadogo chini ya mwaka 1 Wilaya ya Ukerewe

Vifo vya watoto	2014		Jumla Kuu
	Me	Ke	
Chini ya mwaka 1	7	11	
Jumla	**7**	**11**	**18**

Chanzo: Utafiti 2015

Jedwali Na 17: Vifo vya watoto wadogo chini ya mwaka 1 Wilaya ya Mtwara Vijijini

Jina la kituo	Jinsi		Jumla
	Me	Ke	
Kituo cha Afya ya Msimbati	5	6	11
Zahanati ya Msanga Mkuu	0	0	0
Zahanati ya ziwani	1	1	2
Kituo cha Afya cha Mpapura	0	2	2
Kituo cha Afya cha Mahurunga	5	1	6
Kituo cha Afya cha Likomba	0	0	0
Kituo cha afya cha Madimba	0	0	0
Zahanati Ufukoni	0	0	0
Jumla	**11**	**10**	**21**

Chanzo: Utafiti 2015

Jedwali Na 18: Vifo vya watoto wadogo chini ya mwaka 1 Wilaya ya Misungwi

Jina la kituo	Me	Ke
Kituo cha Afya cha Misasi	0	3
Kituo cha Afya cha Koromije	0	0
Zahanati ya Idetemya	0	0
Zahanati ya Ibomgoya	0	1
Jumla	**0**	**4**

Chanzo: Utafiti 2015

Hii ndiyo hali halisi iliyopo katika vituo vingi vya afya na zahanati zilizotembelewa na TCDD. Vifo vya watoto wadogo ambao hawajatimiza mwaka mmoja vimekuwa ni tishio kubwa. Jitihada za ziada zinahitajika ili kupunguza vifo hivyo kutoka vifo 51 kwa watoto 1000 waliozaliwa hai yaani (51/1000) katika mwaka 2009/2010 hadi kufikia vifo 38/1000 kufikia mwaka 2015 kama ilivyokusudiwa. Pamoja na kwamba mpango huu unaishia mwaka 2015 bado serikali inaweza kupunguza vifo hivi kwa kuwa na mipango thabiti yenye kutekelezeka ili kuondoa tatizo hilo.

5.2. Miundombinu ya Afya

Baadhi ya vituo vya afya na zahanati miundombinu yake sio ya kuridhisha. Miundombinu duni huchangia kuwakatisha tamaa wafanyakazi wa sekta hiyo hivyo kuzorotesha huduma inayotolewa katika eneo husika.

Picha 7: Nyumba ya Muuguzi: Kituo cha Afya Msimbati

Chanzo: Utafiti, 2015

Wodi ya wazazi Kituo cha Afya Nagaga Masasi

Huduma bora hutolewa katika mazingira na miundombinu bora, hivyo tunaishauri serikali kuendelea kutenga fedha za kutosha ili kuboresha miundombinu katika sekta ya afya.

5.3. Vifo vya watoto chini ya miaka 5

Mpango wa MKUKUTA wa awamu ya pili ni kupunguza vifo kutoka 81 kwa watoto walio hai 1000 yaani (81/1000) mwaka 2009/2010 hadi 54 kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa hai (54/1000) kufikia mwaka 2015. Je hali ipoje katika ngazi za kutolea huduma?

Jedwali Na 19: Vifo vya watoto wadogo chini ya mwaka 1 Wilaya ya Urambo

No	Vifo vya watoto wadogo chini ya miaka 5, Mwaka 2014		
	Jina la Kituo	**Jinsi**	
		Me	**Ke**
1.	Hospitari ya Urambo	68	52
2.	Zahanati ya Uyumbu	6	10
3.	Zahanati ya Iundu	4	9
4.	Zahanati ya Usisya	11	5
5.	Zahanati ya Mungano	6	3

Chanzo: Utafiti 2015

Jedwali Na 20: Vifo vya watoto wadogo chini ya mwaka 1 Wilaya ya Morogoro Vijijini

Mwaka	**2014**				
Kata	**Mikese**	**Gwata**	**Kiloka**	**Mkambalani**	**Wilaya**
Chini ya miaka 5	00	00	00	00	190
Jumla	**00**	**00**	**00**	**00**	**190**

Chanzo: Utafiti 2015

Jedwali Na 21: Vifo vya watoto wadogo chini ya mwaka 1 Wilaya ya Iramba

Vifo vya watoto	Hospitali ya wilaya		Zahanati ya kinambeu		Zahanati ya Misigiri	
Jinsi	**Me**	**Ke**	**Me**	**Ke**	**Me**	**Ke**
Chini ya miaka 5	6	9	0	0	1	0
Jumla	**6**	**9**	**0**	**0**	**1**	**0**

Chanzo: Utafiti 2015

Jedwali Na 22: Vifo vya watoto wadogo chini ya mwaka 1 Wilaya ya Mtwara Vijijini

Jina la kituo cha Afya	**Jinsi**		**Jumla**
	Me	**Ke**	
Kituo cha Afya cha Msimbati	1	1	2
Zahanati ya Msangamkuu	1	2	3
Zahanati ya Ziwani	1	1	2
Kituo cha Afya cha Mpapura	1	1	2
Kituo cha Afya cha Mahurunga	0	3	3
Kituo cha Afya cha Likombe	1	1	2
Kituo cha Afya cha Madimba	0	0	0
Zahanati ya Ufukoni	0	0	0
Jumla	**5**	**9**	**14**

Chanzo: Utafiti 2015

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliweza kupunguza vifo vya watoto wadogo chini ya umri wa miaka 5, kutoka idadi ya vifo 166 vilivyokuwa vikitokea kwa kila akinamama 1,000 wanaojifungua mwaka 1990 na kupungua hadi kufikia idadi ya vifo 54 kwa kila akinamama 1,000 mwaka 2012. Hii ikiwa ni ndani ya utekelezaji wa mpango wa MKUKUTA II. Pamoja na kuwepo kwa taarifa hizi za kutia matumaini bado tatizo ni kubwa na uwekezaji mkubwa katika sekta hii ya Afya unatakiwa ili kupunguza vifo hivi.

Nchini Tanzania, vifo vya watoto wachanga vinachangia hadi asilimia 40 ya vifo vyote vya watoto walio chini ya umri wa miaka mitano (kwa mujibu wa UNICEF). Sababu zinazopelekea kuwepo kwa tatizo hili ni pamoja na maambukizi ya magonjwa wakati wa ujauzito, malaria, maambukizi ya virusi vya UKIMWI kutoka kwa wazazi, kuzaliwa na uzito mdogo, pamoja na mimba za utotoni.

Kimsingi, vingi kati ya vifo hivi vya watoto wachanga vinaweza kuepukika kwanza kwa kuunganisha nguvu kwa pamoja kati ya serikali, jamii husika, pamoja na wadau mbalimbali. Mimba za utotoni na wazazi kukubali wito wa serikali wa kutukia vyandarua unaweza kutekelezeka na wananchi wenyewe. Pia serikali inapaswa kuboresha huduma za mama na mtoto katika vituo vya kutolea huduma hizo lakini pia kwa kuwa na wataalamu walio na taaluma toshelevu na vifaa tiba vya kutosha vinavyoendana na wakati.

5.4. Mapendekezo ya TCDD

TCDD kama wadau wa maendeleo tunapendekeza serikali iendelee kuimarisha na kuboresha hospitali, vituo vya afya na zahanati ili viweze kutoa huduma bora na kwa wakati sahihi bila kujali mazingira na maeneo yaani mijini au vijijini.

TANZANIA COALITION ON DEBT AND DEVELOPMENT (TCDD)
Shaurimoyo Road, Ilala Area
Mariam Tower, 7th Floor
P.O. Box 80147, Dar es Salaam, Tanzania

Tel: +255 22 2866866
Mobile: +255 736 502661
E-mail: ttcdd@yahoo.com **or** info@tcdd.or.tz
Website: www.tcdd.or.tz